Ukweli wa Mambo

Toleo la Pili la Kauli ya nguvu ya Hoja | Ndugu **Mwandawiro Mghanga** | Juni – Julai 2007

Ndiyo, pamoja tunaweza kuboresha mambo na maisha Wundanyi

Wapinzani wangu wanazurura Wundanyi usiku na mchana wakidai kwamba mimi Mwandawiro Mghanga ni mbunge asiefaa. Kwamba wao watakuwa wabunge bora zaidi kuniliko. Mara ati sistahili kuwa kiongozi, mara sijafanya kitu chochote tangu nichaguliwe. Siwalaumu, kwa vile wanakikamia kiti wako tayari kunichafulia jina kwa kueneza uongo. Wamesahau kwamba mkamia maji hayanywi.

Niliomba kiti cha ubunge cha Wundanyi kwa unyenyekevu bali pia kwa ukakamavu. Nanyi mkakubali mkanipatia fursa ya kuwatumikia. Nayo kazi mliyonipatia ninaitilia manani sana, ninaiheshimu, ninaifanya kwa uaminifu, ari na bidii.

Aidha, uongo hauwezi kugeuka ukweli na ukweli ukawa uongo. Ilivyo pia ni kwamba watu wa Wundanyi wana macho wanaona na vilevile wana masikio wanasikia. Tena wanafahamu tulikotoka, tulipo na tunapokwenda. Pia wanaelewa mimi ni nani na sera zangu wanazijua maana niko nao kila wakati. Isitoshe, vatu wa Wundanyi wanajulikana Taita-Taveta, Pwani na Kenya nzima kwa msimamo wao wa siasa ya nguvu ya hoja. Hata hivyo, si vibaya kukariri ukweli wa mambo. Maana penye ukweli uongo hujitenga.

Niliomba kiti cha ubunge cha Wundanyi kwa unyenyekevu bali pia kwa ukakamavu. Nanyi mkakubali mkanipatia fursa ya kuwatumikia. Nayo kazi mliyonipatia ninaitilia manani sana, ninaiheshimu, ninaifanya kwa uaminifu, ari na bidii. Ndiyo, ninaweza kuwa nimefanya makosa hapa na kule, inawezekana hata nimewaudhi watu wengine kwa njia moja au nyingine, na bila shaka sijatimiza matarajio ya kila mtu. Bali mimi ni binadamu wala siyo Mungu. Ni Mungu pekee ambae ni mkamilifu, binadamu yoyote yule hawezi kukosa unyonge. Pamoja na haya nimejaribu kutimiza wajibu wangu kwa watu wa Wundanyi na Kenya kwa kiasi cha uwezo wangu wote, kama binadamu.

Si uongo nikisema nimewawakilisha ipasavyo bungeni. Sauti ya mbunge wa Wundanyi imekuwa ikisikika bungeni kila mara kwa maswali kuhusu mambo mbalimbali ya eneo bunge letu na kitaifa, na vilevile katika michango ya mijadala, hoja na miswada inayowasilishwa bungeni. Isipokuwa tu nikiwa nje kwa shughuli za kibunge au za eneo bunge la Wundanyi, sikosekani bungeni. Wakati huohuo, niko katika kamati ya bunge inayoshughulikia mambo ya ulinzi na mashauri ya nchi za nje. Kazi hii nimeitekeleza vyema pia. Ndiyo kwa maana nikatajwa kuwa mbunge anaeongoza kwa kushiriki vizuri zaidi katika kazi za bunge. Na huu ni ukweli wa mambo.

Ni ukweli wa mambo pia kwamba tangu niwe mbunge demokrasi imekua na kunoga Wundanyi.

Mikutanoni mimi sizungumzii watu bali ninazungumza na watu, tunaulizana maswali hadharani, tunakosoana, tunajadiliana,

Kwa msingi wa kuhakikisha kuwa hakuna mtu au sehemu itawachwa nyuma kimaendeleo, ninahakikisha ninatembelea kila lokesheni mara kwa mara. Nimefika subulokesheni zote za Wundanyi tena mara nyingi.

Upandaji wa miti kuhifadhi mazingira, Kishushe.

tunashauriana. Ninawasikiliza watu nao wananisikiliza. Ni siasa kali lakini za heshima bila chuki. Nikizungumza ninafanya maksudi ya kusema ukweli, ya kuelimisha watu, ya kueneza siasa ya nguvu ya hoja. Si uongo nikisema kuwa watu wa Wundanyi ni baadhi ya watu wenye mwamko wa kisiasa zaidi nchini. Aidha, wako pamoja na wale wanaoongoza nchini kwa kutambua haki zao na katika kushiriki katika kueleza hisia zao na kuamua kuhusu miradi yao ya maendeleo. Ndiyo kwa sababu hata miradi ya pesa za mfuko wa maeneo bunge inaamuliwa na kutekelezwa kwa haraka zaidi kuliko maeneo bunge mengine nchini.

Ukweli wa mambo ni kwamba kama si kucheleweshwa ama hata kuhujumiwa na wizara mbalimbali zilizoko chini ya Mkuu wa Wilaya ya Taita – Taveta, tungetimiza mengi zaidi na kwa muda mfupi zaidi katika eneo bunge letu. Pia wanawake wa Wundanyi wana mwamko wa hali ya juu, wako msitari wa mbele katika miradi mingi ya maendeleo na wanashiriki vilivyo katika kutoa hoja na maono. Si ajabu basi kwamba wakati kura za maoni kuhusu katiba zilipopigwa, Chungwa ilishinda Ndizi katika kila kituo cha kupiga kura Wundanyi tena licha ya propaganda zilizokuwa zimefanywa kupitia kwa redio, televisheni na magazeti. **Hili ni dhihirisho kuwa watu wa Wundanyi wameelimika kuhusu katiba, wanafahamu maslahi yao, ya Taita-Taveta na ya kitaifa. Hivyo wanajua kwa nini wanataka katiba yenye msingi wa Bomas, iliyo na usamabazaji wa mamlaka ya utawala hadi mashinani, ikiwa ni pamoja na mfumo wa majimbo.**

Nimejtahidi kuwaunganisha watu wa Wundanyi. Nimekataa siasa za udaku, fitina na masengenyo. Naheshimu haki ya kila mtu ya kutoa maoni yake, hata kunihusu, na kuwa kwa chama anachokipenda. Kwa sababu hii kila mara nasisitiza kuwa nikiwa mbunge ninawakilisha kila mtu hata wapinzani wangu pia. Hivyo katika shughuli za maendeleo nimekuwa nikihusisha kila mtu bila ubaguzi.

Nimehakikisha kuwa lokeshini zetu zote saba, Wumingu, Kishushe, Wundanyi, Mbale, Mgange, Mwanda na Werugha nazitumikia kwa haki na usawa. Katika miradi ya maendeleo ya pesa za mfuko wa maeneo bunge kila lokesheni imefaidi na itaendelea kufaidi.

Kwa msingi wa kuhakikisha kuwa hakuna mtu au sehemu itawachwa nyuma kimaendeleo, ninahakikisha ninatembelea kila lokesheni mara kwa mara. Nimefika subulokesheni zote za Wundanyi tena mara nyingi. Nimeenda mara nyingi hata katika vijiji ambavyo havijawahi kuona mbunge hapo awali kama Funju ya Mwanda, Marungu, Mkamwasi, Mdindonyi ya Mbale, Daku, Paranga, Mbulia, Mlilo, n.k. **Ninatekeleza sera yangu ya kufikia watu pahali walipo ili nijue hali yao, matatizo yao, maoni yao na mapendekezo yao kuhusu miradi ya maendeleo. Kwa ufupi, nimekuwa karibu na watu mashinani tukiunganika na kushirikiana katika harakati za siasa na maendeleo.**

Pia wanawake wa Wundanyi wana mwamko wa hali ya juu, wako msitari wa mbele katika miradi mingi ya maendeleo na wanashiriki vilivyo katika kutoa hoja na maono.

Katika kutekeleza haki zetu za kidemokrasi Wundanyi, tumefefika kiwango cha kudai haki zetu kwa maandamano. Maandamano ya amani ambapo umma unaeleza hisia zao kuhusu mambo yoyote yanayowakera ni haki ya kikatiba na sehemu ya demokrasi. Kwa sababu hii mwaka huu niliongoza maandamano ya watu wa Wundanyi na Taita – Taveta ambayo pamoja na mambo mengine yalilaani kutokuwa na uwazi na uwajibikaji katika afisi za serikali katika makao makuu ya wilaya Wundanyi. Aidha, wakati wa maandamano yenyewe wananchi, wanaume kwa wanawake, wazee kwa vijana, walilaani dhuluma na nyanyaso wanazetendewa na matajiri wanaomiliki ardhi na migodi Chungaunga, Kamtonga, Kishushe na Kasighau. Aidha, maandamano yalitetea haki za watu wa Taita – Taveta za kumiliki na kufaidi kutokana na rasilimali zao za ardhi, mbuga za wanyamapori, madini, maji na misitu. Kwa maandamano hayo tulitangaza wazi na bayana kwamba hatutaendelea kuvumilia kuendelea kuona utajiri tuliyotunukiwa na Mwenyezi Mungu ukifaidi watu wachache, wengi kutoka nje ya Taita – Taveta, huku tukiishi kwa ufukara na kudharauliwa. Ilikuwa ni kupeleka demokrasi kwa ngazi ya juu zaidi ya kudai mambo halisi yatakayoboresha maisha ya wakaazi wa wilaya ya Taita - Taveta. Mapambano haya yataendelea mpaka yafaulu, wapinzani –wapende wasipende, huu ni mwanzo tu. Ikiwa

nitachukiwa na yoyote yule kwa msimamo huu, niko tayari. **Kwani nilichaguliwa kuwakilisha masilahi ya watu wa Wundanyi wala siyo wadhalimu na wafisadi wa mali ya umma popote walipo. Isitoshe, mlichagua shujaa wa harakati za ukombozi, wala siyo kibaraka au mwoga. Kwani nchi haitakombolewa na waoga wa kujipendekeza kwa wenye uwezo na wanaotumia mamlaka vibaya.** Uongozi ni kumulikia umma njia ya ukombozi na vilevile kuwa katika msitari wa mbele wa mapambano yao.

Hebu sasa tutazame historia ya Eneo Bunge letu la Wundanyi ili tukumbuke tulipotoka, tulipo na tumulike huko tunapokwenda. Mlinichagua kuwa mbunge wenu mnamo Disemba mwaka wa 2002 na nikaanza kazi rasmi bunge lilipofunguliwa mnamo mwaka wa 2003.

Nikiwa mbunge nilichangia katika kutengeneza Sheria ya Pesa za Mfuko wa Maeneo Bunge pamoja na wabunge wenzangu. Hata serikali ilipositasita kutekeleza sheria yenyewe nilishirikiana na wabunge wengine kuishinikiza ianze kutekeleza sheria yenyewe. Tulikubaliana kama wabunge kwamba bila Wizara ya Fedha kuonyesha nia kwa vitendo halisi vya kutekeleza sheria ya CDF, hatutapitisha bajeti ya kitaifa na hivyo serikali itaanguka. Ikawa haina budi ila kufanya kama tulivyodai na ndipo kiasi cha milioni

...ndiyo kwa maana nikatajwa kama mbunge anaeongoza kwa kushiriki vizuri zaidi katika kazi za bunge

sita kikatengewa kila eneo bunge nchini kama dalili ya nia ya serikali ya kuanza kutekeleza mpango huu mwafaka ambao umefaulu kuharakisha maendeleo kote nchini, hasa mashambani. Sasa kila mwaka asilimia mbili nukta tano (2.5%) ya jumla ya kodi zinazokusanywa kila mwaka hugawanywa kwa kila eneo bunge nchini ili kufanya miradi ya maendeleo inayopendekezwa na pia kusimamiwa na wananchi wenyewe mashinani.

Katika toleo lingine la *Ukweli wa Mambo* nitachambua kwa marefu na mapana kuhusu jinsi Pesa za Mfuko wa Maeneo Bunge (CDF) zinavyotumika Wundanyi. Bali wananchi wenyewe mnaelewa maana nyinyi wenyewe ndiyo mnaotekeleza miradi yenu. Isitoshe, tunakutana kila mara maana ninahakikisha kuwa mimi mwenyewe ninaifuatilia na kuikagua miradi yenyewe moja kwa moja. Tena mnakumbuka kuwa kila mara nawakumbusha ukweli kuwa Pesa za Mfuko wa Maeneo Bunge si za Mwandawiro bali ni kodi zenu wenyewe na hakuna mtu ambae halipi kodi. Pia huwa ninawaeleza kuwa mlikuwa mnalipa kodi kila mara lakini CDF haikuwepo. Ilihitaji bunge la sasa kumkombolea sehemu kidogo ya pesa zenu, na tena tunadai ziongezwe maana ni haki ya wananchi.

Nilikuta barabara zimeharibika mno. Wakati mvua iliponyesha magari hayangeweza kusafiri kutoka Wundanyi hadi Werugha, Mgange, Mbale, Mwanda, Mghambonyi au Nyache, kwa mfano. Na ingawa sijatosheka kwamba zimekuwa nzuri haizuru barabara nyingi Wundanyi zinapitika mwaka mzima, kuwe

Shule za msingi

Nilipoingia bunge nilikuta shule zetu, hasa za msingi, zikiwa katika hali mbaya mno. Pahali pengine kama Mlilo, na sehemu zingine za Wumingu hata hapakuwa na shule kabisa. Hapakuwa na madarasa wala madawati. Ndiyo kwa maana matokeo ya mtihani yalikuwa yakizorota Wundanyi kila mwaka. Sasa tumekarabati shule na kuletea madawati karibu shule zote Wundanyi na tunaendelea na kazi hii. Zingine tumeanza kuzibomoa na kuzijenga upya. Vilevile, tunaanzisha shule mpya pahali zinahitajika kama Funju ya Mwanda na Daku ambako watoto wanalazimika kwenda mbali mno kila siku kushiriki shule. Tunarekebisha na kujenga hata nasari. Tunatarajia kuwa matokeo ya mtihani yataendelea kuboreka.

Hata shule za upili hazikuachwa nyuma ingawa tulitilia manani zaidi shule za msingi kwani zilikuwa katika hali mbaya zaidi. Tumefaulu hata kufungua shule mpya mbili za upili, Funju Secondary School iliyoko Shagha na Mbela Secondary School kule Kishushe.

Wanafunzi wa shule ya msingi ya Mwanyalo, Wumingu. Sasa tunawajengea shule ya ghorofa

kumenyesha au hakujanyesha. Pia kupitia kwa juhudi za wananchi zinazotiwa motisha na mpango wa CDF niliouanzisha wa wananchi katika vijiji kujenga barabara zao wenyewe huku wakijipatia hela kidogo, tumekarabati barabara kadhaa katika kila lokesheni na kufungua zingine mpya kabisa. Aidha, tumejenga madaraja na tunazidi kutenga pesa ili kujenga madaraja kila yanapohitajika Wundanyi.

Nilipoingia bunge nilikuta karibu miradi yote ya maji Wundanyi imekwama au haikuwepo kabisa. Leo tumefufua karibu miradi yote ya maji katika Eneo Bunge letu na tukaanzisha mipya pia. Idadi ya watu Wundanyi ambao wanakunywa maji ya mifereji imeongezeka tena kwa ukubwa. Na bado tunaendelea na kazi hii yenye lengo la kuhakikisha tunahifadhi mazingira na chemichemi za maji huku tukijitahidi kuwapelekea watu maji masafi karibu na walipo. Ninatambua kuwa maji ni uhai.

Nilikuta dipu za kuogesha mifugo karibu sehemu zote za Wundanyi zimekufa. Kwa kuzikarabati na kuzipa dawa ya kuanzia tumefufua dipu zote Wundanyi. Kilichobaki ni kampeni ya kuwashiwishi wakulima wa mifugo waziendeleze dipu zao kwa kutibu mifugo yao mara kwa mara. Aidha, tuna mipango ya kuanzisha dipu mpya pahali zinapohitajika na vilevile kushirikiana na wakulima kuleta mbegu za ng'ombe bora wakutoa maziwa mengi zaidi.

Kutokana na maombi niliyopeleka kwa Mamlaka ya Bandari ya Kenya (KPA) tumejenga na tutafungua kituo cha afya cha Sangeroko cha kuwahudumia watu wa Mwaroko na Sangenyi. Isitoshe, tumekamilisha na tutafungua kituo cha afya cha Mgange Dawida kilichoanzishwa na wananchi miaka mingi iliyopita. Vilevile, miradi ya umeme inaendelea Sangenyi – Mwaroko hadi Kishushe, Shagha – Funju, Shigharo, Mgange Dawida na Ngulu. Kama sehemu zingine nchini, watu wanahitaji umeme na miradi ya umeme haitekelezwi kwa kasi inayohitajika. Bali inaendelea na nina hakika wakati haupo mbali ambapo kila mtu Wundanyi atakuwa na umeme.

Aliekuwa Waziri wa Utangazaji na Mawasiliano, Rafael Tuju, tukiwa Werugha Multipurpose Hall, 2004

Nilipoingia bungeni hapakuwa na simu za mkono wala televisheni haikuwa inaonekana Wundanyi. Lakini leo baada ya kumleta aliekuwa Waziri wa Utangazaji na Mawasiliano, Rafael Tuju, Wundanyi, na kueleza haya yote ya wizara yake, sasa kuna simu za mkono na watu wanaona televishini, hata kama ni KBC peke yake.

Tumetaja machache tu kuhusu historia yetu ya maendeleo. Wala hatuwezi kutaja kila kitu tunachofanya. Kwa mfano, hatujataja kuhusu majumba ya mikutano tunayokarabati, kujenga na kupanga kujenga. Kwa mfano, mradi wa Werugha Multi-purpose Hall uliokufa kwa miaka mingi sasa umefufuka.

Tunatarajia kukarabati na kujenga majumba ya mikutano katika kila lokesheni na sabulokesheni. Tena kila jumba litakuwa na fanicha, televisheni ya satelaiti, video na vifaa mbalimbali. Majumba haya tunayoyajenga na kutengeneza ni sehemu ya kukuza demokrasi na kujumuisha watu kwa ajili ya maendeleo, shughuli za kijamiii na kitamaduni.

Kwa muhtasari, Wundanyi haijalala kimaendeleo katika kipindi changu cha ubunge. Ninawashukuru watu wa Wundanyi kutoka kila sehemu, hasa viongozi wa miradi mbalimbali, kwa juhudi zenu na kwa kujitolea kwenu kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo. Ninajivunia kila wakati kwamba watu wa Wundanyi wako mbele sana katika kushiriki kimaendeleo na kwa haraka ya kutambua mahitaji yao ya maendeleo. Hii inafanya kazi yangu kama mbunge wenu kuwa raisi zaidi.

Ukweli wa mambo ni kuwa ninahitaji miaka mingine zaidi kwani tunahitaji tuendelee kushirikiana na kufanya kazi pamoja kukamilisha miradi tuliyoianzisha.

Kwa kipindi hiki cha miaka mitano ambacho kiko karibu kufika ukingoni, tumeonyesha dalili kuwa tunaweza kuboresha mambo na maisha Wundanyi. Ninawapenda, napenda maendeleo tena napigania ukweli, haki na demokrasi kwa ushujaa, na Kenya nzima inatambua hili. Hivyo basi, sitachoka kuendelea kuwasihi muendelee kuniunga mkono ili pamoja tuendelee kubadilisha Wundanyi, Taita na Kenya kwa uzuri.

KAENYI PANANA NA SERE YA MLUNGU KARI KOSE!!!

CONTACT: Telephone: 254 – 20 – 2848540 Ext. 32540 Email: mwandawiro2002@yahoo.com